Mater
Health Services Brisbane Limited

Swahili

HEALTH CHECKS ON ARRIVAL IN AUSTRALIA (Swahili)

UCHUNGUZI WA AFYA WAKATI KUWASILI NCHINI AUSTRALIA

Maelezo msingi (Background)

- Watu wengi wanaokuja nchini Australia wameshakuwa na shida ya kufikia huduma za afya pale ng'ambo
- Matatizo ya afya yanaweza kusababishwa na kukosa chakula lishe bora, hali ya maisha na maji machafu
- Pia watu wanaweza kuwa na matatizo ya afya yenye mhemuko inayosababishwa na vita, kupoteza ndugu/jamaa na marafiki, na matendo dhidi ya haki za binadamu.

Uchunguzi wa afya kabla ya kusafiri (Pre-travel health checks)

- Watu wengine wameshapata uchunguzi wa afya kabla ya kuwasili, na wanakuwa wameshapimwa kwa ajili ya HIV, kifua kikuu na magonjwa mengineo kama homa ya mbu
- Watu wengine wanaweza pia wameshapata matibabu ya minyoo, na chanjo ya surua, ugonjwa wa
- matubwitubwi na surua ya rubella
- Mara nyingi uchunguzi wa afya kabla ya kusafiri umeshafanywa miezi mingi kabla ya kusafiri, na kuna
- uwezekano kupata shida ya afya baada ya kupata majibu. Kwa sababu ya hii, vipimo vingine vinaweza
- kurudiwa tena baada ya wewe kuwasili nchini Australia.

Mbona ufanyiwe uchunguzi wa afya baada ya kuwasili nchini Australia?
(Why have a health check after you arrive in Australia?)

- Huu ni hatua muhimu katika kuboresha afya yako unapowasili nchini Australia kwa sababu uchunguzi
- unaweza kugundua matatizo ya afya ambayo hukuyafahamu
- Kama ugonjwa wowote ukigunduliwa, utapewa matibabu kama ikihitajika
- Mfanyakazi wa afya anaweza kukuelekeza kwenye zahanati ya bingwa kwa ushauri zaidi, au kwa huduma kama vile huduma za afya ya wanawake, afya ya meno na macho, na ushauri nasaha.

Uchunguzi wa afya unahusu nini? (What the health check involves)
Uchunguzi wa afya unaweza kuendelea kwa muda wa saa moja au zaidi, na unaweza kuhusika na mambo yafuatayo:

- Maswali kuhusu afya yako
- Uchunguzi wa kimwili
- Kukusanya sampuli za damu, mkojo na choo
- Chanjo.

Mfanyakazi wa afya anaweza kukuuliza kama una matatizo yoyote yanayoweza kuhusika na matukio kwako kabla ya kuwasili. Kunazo huduma maalum zinazoweza kukusaidia kuwezana na maswala hayo. Wakati mwingine unaweza kuhitaji kutembelea zahanati au ofisi ya dakati zaidi ya mara moja.

Chanjo ni mhimu (Vaccination is important)

- Kuandikisha mtoto wako katika shule na huduma ya kulea watoto, mtoto wako atahitaji kuchanjwa kikamilifu. Shule inaweza kukataa kumupokea kama mtoto wako hajapata chanjo, au hajaanza utaratibu wa chanjo. Kujiandikisha katika madarasa ya Watu wazima ya Kiingereza katika TAFE, utahitaji pia kuweza kupata chanjo
- Kama mtoto wako amekamilisha chanjo zao wanaweza kuhitaji barua ya uthibitisho kutoka kwa daktari wao kueleza hili.
- Ni lazima kuhakikisha mtoto wako anamaliza utaratibu wa chanjo.
- Ili kupokea malipo ya Centrelink, mtoto wako anahitaji chanjo kikamilifu.

Wakati watu wamepata chanjo inafaidisha jamii nzima.

Unafaa kuleta nini nawe? (What should you bring with you?)

- Kadi ya Medicare, au nambari ya Medicare, kama ikipatikana
- Kumbukumbu ya chanjo na maelezo kuhusu historia yako ya afya.

Nini hutokea baada ya uchunguzi wa afya? (What happens after the health check?)

Mfanyakazi wa afya anaweza kukuomba kurudi tena Wakati majibu ya vipimo yanapokuwa tayari. Hivi ni ili kupanga matibabu na kufuatilia kama ikihitajika.

Usiri (Confidentiality)

- Uchunguzi wa afya ni bure na ya siri, na hauathiri hali yako ya mkaazi nchini Australia
- Majibu yote ni ya siri, na hayawezi kupatiwa watu wasiohusika na utunzaji wa afya yako bila ya ruhusa yako. Wafanyakazi wa afya hawaruhusiwi kuzungumza kuhusu matatizo yako ya afya na yeyote, ila Wafanyakazi wengine wa afya wanaohusika na utunzaji wako.

Wakalimani (Interpreters)

Kama Kiingereza sio lugha yako ya kwanza, mkalimani anaweza kukusaidia kuongea na Wafanyakazi wa afya pamoja na kupata huduma nzuri sana.Tafadhali omba mfanyakazi wa afya akupangie mkalimani, au apigie simu Huduma za Mkalimani wa Simu kwa nambari ya 131 450.

Maelezo zaidi Kwanye lugha ya kiswahili yanapatikana kutoka kwenye
www.communityhealthhub.com.au **(Further health information in Swahili is available from)**

Thanks to South Eastern Sydney Illawara NSW Health for this information and translation.